**AckySHINE.com**

# Amri ya nne ya Mungu: Kuheshimu Wazazi

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · December 19, 2016

Mafundisho ya Katekisimu · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Amri za Mungu

Katika Amri ya nne ya Mungu tumeamriwa nini?

Tumeamriwa tuwaheshimu wazazi wetu na wakubwa wetu wote, tuwapende, tuwatii na tuwaombee. (Kut 20:12, Kol 3:20)

Amri ya Nne ya Mungu tumeamriwa nini?

Tumeamriwa tuwaheshimu wazazi wetu na wakubwa wote, tuwapende, tuwatii na tuwaombee. (Kut 20:12), Kol 3:20

Kwa sababu gani yatupasa kuwaheshimu Baba na Mama?

Yatupasa kuwaheshimu Baba na Mama kwa sababu;

1. Wameshirikiana na Mungu kutuleta duniani walipotuzaa 2. Wamewekwa na Mungu ili watulee na kutuongoza Mbinguni 3. Mungu ameamuru tuwapende wazazi mara baada ya Yeye. (Ayu 3:1-9)

Wazazi na wakubwa wameamriwa nini?

Wazazi na wakubwa wameamriwa watutunze na kutulea

Tuwaheshimu Baba na Mama kwa matendo gani?

Tuwaheshimu Baba na Mama kwa matendo ya adabu, heshima, utii na mapendo (Ayu 3:12)

Twawakosea Heshima Baba na Mama kwa kufanya nini?

Twawakosea Heshima Baba na Mama kwa;

1. Tukiwakasirisha na kuwatukana 2. Tukiwakaidi na kuwapiga 3. Tukiacha kuwaombea 4. Tukiacha kuwasaidia katika shida na uzee. (Kut 21:15-17)

Wazazi wawaleeje watoto wao katika imani ya Kikristo?

Wawalee hasa kwa mfano wao, kwa sala, kwa katekesi ya kifamilia na kushiriki maisha ya Kanisa

Lini tunakatazwa kuwatii watu?

Tunakatazwa kuwatii watu wanaotuamuru jambo lililokatazwa na Mungu (Mdo 5:29)

Katika Amri ya Nne ya Mungu tumekatazwa nini?

Tumekatazwa haya;

1. Kukaidi wazazi na wakubwa wetu 2. Kuwakasirisha. 3. Kuwadharau.

Wakubwa tunaopaswa kuwaheshimu ni kina nani?

Wakubwa hao ni;

1. Viongozi wa Kanisa 2. Viongozi wa Serikali 3. Walimu na walezi 4. Wakubwa wa kazi (War 13:1) 5. Viongozi wa Jumuiya